



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA SINGIDA



Mkoa wa Singida.
Simu Na. 0262502252/2237
Fax Na. 0262502719
Barua pepe: ded.singidadc@singida.go.tz

S.L.P. 27,
SINGIDA.

Kumb. Na. SDC/B.1/50/PART C/98

Tarehe: 01/11/2023

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI ZA MKATABA

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya Singida anawatangazia wataanzania wenye sifa na nia ya kufanya kazi katika Halmashauri ya Wilaya Singida, kuomba nafasi ya kazi ya mkataba wa mwaka mmoja kama ifuatavyo:

DEREVA DARAJA LA II (Nafasi 4)

1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

- i. Awe na elimu ya Kidato cha Nne (IV) au sita (VI).
- ii. Awe na Leseni ya Daraja "E" au "C1" ya uendeshaji wa Magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (1) bila kusababisha Ajali.
- iii. Awe amehudhuria Mafunzo ya msingi ya uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

1.2 KAZI/ MAJUKUMU YA DEREVA DARAJA LA II

- i. Kukagua Gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa Gari.
- ii. Kuwapeleka Watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.
- iii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya Gari.
- iv. Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali.
- v. Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari
- vi. Kufanya usafi wa Gari.
- vii. Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake wa kazi.

1.3 MSHAHARA

- i. Ngazi ya Mshahara ni TGS A 1.

2.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI


- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri kuanzia miaka 18 hadi 45.
- ii. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa.

- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed C.V) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya wadhamini (referees) wawili
- iv. Maombi yote yaambatane na picha 1 (passport size), nakala za vyeti vya taaluma vyeti vya kidato cha nne na kidato cha sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa zilizoolekezwa hapo juu.
- v. Waombaji wote waambatanishe nakala ya kitambulisho cha Taifa (NIDA) kwa ambao hawana vitambulisho hivyo, namba za nida ziandikwe kwenye maelezo binafsi (CV).
- vi. "Testimonials", "Provisional Results", "Statement of results", hati matokeo za kidato cha nne na sita (FORM IV AND FORM VI RESULTS SLIPS) **HAVITAKUBALIWA.**
- vii. Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (TCU au NECTA).
- viii. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wanakibali cha Mamlaka husika.
- ix. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**
- x. Maombi yote yatumwe kwenye anuani ifuatayo;

Mkurugenzi wa Mtendaji
Halmashauri ya Wilaya,
S.L.P 27,
SINGIDA.

N:B Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 09 Novemba, 2023 saa 9.30 alasiri.

Imetolewa na


Ester Chaula
MKURUGENZI MTENDAJI
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA

**MKURUGENZI WA
HALMASHAURI YA WILAYA
SINGIDA**

Nakala: Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya Singida
Singidadc.go.tz

Mbao za Matangazo